# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA

**26 AGOSTI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 26 AGOSTI, 2026

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA:**

**III. TAMKO LA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE WOTE:**

**IV. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**1. MHESHIMIWA AISHA MSANTU MDUYAH (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa vyumba viwili vya Maabara katika Shule ya Sekondari Msakwalo iliyopo Kata ya Ovada Wilayani Chemba.

**2. MHESHIMIWA ENG. KIJA LIMBU NTEMI (KATORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, hatua gani zinahitajika ili kupatiwa Halmashauri Jimbo la Katoro na Busanda ambayo yamekidhi vigezo vya kuwa na Halmashauri.

**3. MHESHIMIWA MARIRTA GIDO KIVUNGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya cha Mfereji ikizingatiwa kuwa fedha za ujenzi zilitengwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**4. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (ITWANGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Didia ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa Wananchi wa eneo hilo.

## WIZARA YA NISHATI:

**5. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha kazi ya kupeleka Umeme katika Vijiji vya Wilaya ya Kwimba, hususani Vijiji vya Ng'wambogwa na Kawekamo.

**6. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASINI CHIKAMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Umeme kwenye Vitongoji visivyo na Umeme Wilayani Tunduru.

## WIZARA YA MAJI:

**7. MHESHIMIWA CHARLES MHANDO NJAMA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Korogwe Mjini wataanza kupata Maji kutoka kwenye Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**8. MHESHIMIWA ASHA RAMADHAN BARAKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaunda Tume itakayotatua migogoro ya ardhi nchi nzima.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**9. MHESHIMIWA MARYAM USSI YAHYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha uhai na uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa malipo ya michango ya nchi Wanachama yanasuasua.

**WIZARA YA MADINI:**

**10. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOSEPH KAPOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itaruhusu Wananchi kupewa vibali vya kuchimba Madini kwenye Hifadhi.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**11. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka mitandao ya simu na intaneti Kata za Ruaha, Sali, Vigoi, Kichangani, Iragua, Ilonga, Mbuga na Euga – Ulanga.

**WIZARA YA VIWANDA:**

**12. MHESHIMIWA ASHA OMAR RASHID (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia masoko ya Mwani Wakulima wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**WIZARA YA KILIMO:**

**13. MHESHIMIWA PASCHAL INYASI CHINYELE (DODOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Mabwawa ya Umwagiliaji katika Kata za Mbabala, Mpunguzi, Matumbulu na Mbalawala ili Vijana waweze kujihusisha na kilimo.

**14. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani kuwalinda Wakulima wadogo wenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa Miradi ya Umwagiliaji  Mkombozi na Pawaga Iringa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**15. MHESHIMIWA HAIDARY HEMED SUMRY (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza riba ya Mikopo ya biashara kwenye Mabenki ili kuwawezesha Wafanyabiashara kulipa Mikopo kwa wakati.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**16. MHESHIMIWA RASHID MOHAMED MTIMA (NEWALA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga Josho la kuogeshea mifugo katika Jimbo la Newala Mjini.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**17. MHESHIMIWA MOHAMMED KASSIM SALUM (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa kuhakikisha Polisi wote nchini wanakuwa na vitendea kazi *Radio Calls* na kompyuta ili kurahisisha mawasiliano.

**18. MHESHIMIWA IMAMU MTUMWA VUAI (MAGOMENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa kuimarisha Idara ya Uhamiaji kutumia teknolojia za kisasa za utambuzi na udhibiti wa mipaka ili kuimarisha usalama.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**26 AGOSTI, 2026** **KATIBU WA BUNGE**